*Kioo cha Lugha, Juz. 22(2), 211-228*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v22i2.4

# Tofauti za Kifonolojia na Kimsamiati baina ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili Sanifu

*Ahmad Y. Sovu*[1]

**Ikisiri**

Watanzania wengi, hususani waishio vijijini, wana lugha zao za asili ambapo hujifunza Kiswahili na kukitumia kama lugha ya pili. Watanzania hao, wanapotumia Kiswahili huonekana wakibadili baadhi ya sauti na maneno. Makala hii inalenga kuchunguza tofauti za kifonolojia na kimsamiati baina ya Kiswahili cha Kigoma Ujiji na Kiswahili sanifu ili kubaini tofauti za matumizi ya sauti na maneno kati ya lugha hizo. Data zimekusanywa kwa kutumia ushuhudiaji na majadiliano ya vikundi. Uchambuzi na uwasilishaji wa data umeongozwa na Mkabala wa Mbinu Linganishi (Anttila, 1972). Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa kuna tofauti ya kifonolojia baina Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu katika sauti zenye maneno yenye asili ya kigeni kama vile sauti [h], [bu], [mu]. Pia, kuna tofauti ya mabadiliko ya sauti [a] badala ya sauti [ha], [s] kuwa [sh], [r] badala ya [l], [bh] badala ya [b] na [bu] au [tu] kuwa [wa]. Aidha, kuna tofauti za matumizi ya sauti [-ga], lafudhi na mabadiliko ya kialami [ngo] badala ya sauti [eti] na tofauti za urefushaji irabu. Katika muktadha huo, Kiswahili cha Kigoma, Ujiji kinafanana na kutofautiana na Kiswahili sanifu kifonolojia na kimsamiati. Hata hivyo, tofauti zilizobainika ni zile za ubadilishaji wa sauti na msamiati usio wa msingi katika lugha hizo ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na athari za lugha mama.

## 1.0 Utangulizi

Kiswahili ni lugha ya Kibantu ambayo kwa mujibu wa Massamba (2017) inazungumzwa na watu zaidi ya milioni 150 ulimwenguni. Lugha hii inazungumzwa na zaidi ya watu milioni 100 Afrika Mashariki na Kati pekee. Watu wa Afrika Mashariki na Kati hutumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano mapana. Aidha, Sera ya Lugha ya Tanzania inaeleza kuwa Kiswahili sanifu ni lugha rasmi na lugha ya taifa (Mekacha, 2011). Katika muktadha huo, Kiswahili ni lugha ya mawanda mapana inayotumiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii, nchini Tanzania. Hata hivyo, watu wengi katika sehemu za vijijini hujifunza lugha zao za awali zinazotumika katika jamii zao kabla hawajaanza shule. Wanapoanza

[1] Mhadhiri, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam, Tanzania.
Baruapepe: sovu82@gmail.com

shule, watoto hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili ambapo lugha zao za awali husababisha athari fulani katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Pia, katika jamii hujitokeza athari mbalimbali za lugha za asili zinazoathiri matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili (Nyanda, 2015).

Katika athari hizo, mtumiaji wa lugha ya Kiswahili huhifadhi sifa fulani za lugha yake ya kwanza au huongeza kanuni katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Tafiti zilizofanyika zinaonesha kuwa watumiaji wengi wa Kiswahili wanaoishi vijijini nchini Tanzania, wanatumia Kiswahili kilichoathiriwa na lugha zao za kwanza, hata kama lugha hizo zina uhusiano wa karibu (Wenceslaus, 2015). Kwa mfano, Masebo na Nyangwine (2008) wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za Kibantu ambapo mwingiliano huo umeleta athari katika Kiswahili. Aidha, kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya pili katika jamii nyingi za vijijini, watumiaji wengi wa Kiswahili huonesha athari za lugha zao za kwanza. Athari hizo huonekana zaidi katika viwango vya matamshi, msamiati na maumbo ya maneno.

Tafiti mbalimbali zimekwishafanywa kuchunguza tofauti za usemaji wa lugha ya Kiswahili katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania. Mathalani, Kipacha (2002) alichunguza tofauti ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kipemba, na Khamis (2016) alichunguza tofauti ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu. Katika tafiti hizo walibaini kuwa Kiswahili cha kisiwa cha Pemba kinatofautiana kimatamshi na kimsamiati kutoka eneo moja hadi jingine. Hali hii tunaweza kuiona pia kupitia watumiaji wa mijini na vijijini katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara.

Katika kuthibitisha madai hayo, Massamba (2006) alilinganisha Kiswahili cha Musoma na Kiswahili sanifu huku akitafakari kama huo ni mwanzo wa lahaja nyingine. Katika utafiti huo alibainisha tofauti mbalimbali za kiisimu baina ya lugha hizo. Tofauti hizo zilibainika katika vipengele vya kifonolojia, kimofolojia na msamiati usio wa msingi. Aidha, Massamba (2006) anahitimisha kuwa utafiti zaidi unaweza kufanyika katika maeneo mengine ya Tanzania Bara ili kubaini utokeaji wa tofauti kama hizo. Kutokana hoja hiyo, mwandishi wa makala hii ameshawishika kuchunguza tofauti za kifonolojia na kimsamiati katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu. Sehemu inayofuata inahusu tofauti za watumiaji wa lugha moja.

### 1.2 Tofauti ya Watumiaji wa Lugha Moja

Lugha katika jamii ina mpangilio maalumu wa sauti na maneno unaofuatwa na wanajamii husika ili iweze kutoa ujumbe. Mpangilio huo wa sauti, maneno pamoja na maana zake lazima uwe unaokubalika katika jamii hiyo. Katika jamiilugha moja, watu hutofautiana katika utamkaji kutokana na sababu mbalimbali. Mdee (2004) anafafanua kuwa tofauti za lugha zinaweza kutokana na tofauti za kiuchumi, aina ya kazi wanayoifanya na hata eneo wanaloishi. Kwa mfano, vijana wa vijiweni au wafugaji huwa na msamiati wao wanapokuwa katika kundi lao;

watu wa eneo maalumu pia huongea lahaja ya mahali pale na hata wakiwa nje ya eneo lao hutambulika kutokana na msamiati wanaoutumia na namna wanavyotamka ambavyo huwatambulisha mahali wanakotoka. Gumperz (1968) akirejelewa na Mathooko (2007) anaeleza kuwa kupitia jamiilugha, watu wanatofautiana kwa ishara za kimaongezi katika matumizi ya lugha. Mdee (*keshatajwa*) anaendelea kueleza kuwa tofauti za kiisimu, kama vile kifonolojia, kisarufi na kimsamiati hubainisha lahaja ndani ya lugha moja. Hata hivyo, anaeleza kuwa sababu za kutokea kwa tofauti hizo zinaweza kuwa za kibinafsi, kitarafa, kitabaka, kirejista au kilahaja. Sehemu inayofuata inazungumzia Kiswahili cha Kigoma, Ujiji.

**1.2 Kiswahili cha Kigoma, Ujiji**

Kigoma, Ujiji imo katika Manispaa ya Kigoma Ujiji ambako ndiko Kiswahili cha Kigoma, Ujiji kinapotumika. Kiswahili cha Kigoma, Ujiji huzungumzwa katika maeneo yote ya ndani ya Manispaa ya Kigoma, Ujiji ambayo ni kata za Ujiji, Mwanga, Gungu, Kibirizi na Bangwe. Aidha, kutokana na mwingiliano wa kijamii baina ya wakazi wa Manispaa ya Kigoma, Ujiji na maeneo mengine, mawasiliano hufanyika kwa kutumia Kiswahili ambacho tunaweza kukiita Kiswahili cha Kigoma, Ujiji. Kijiografia, Mkoa wa Kigoma, umepakana na nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Rwanda. Kwa hivyo, huu ni miongoni mwa mikoa ambayo ina mwingiliano mkubwa wa jamii tofautitofauti za ndani na nje ya Tanzania. Kabla ya kuanza kuziainisha tofauti hizo, tutajadili kidogo kuhusu watu waishio Kigoma.

**1.3 Watu Waishio Kigoma, Ujiji**

Mkoa wa Kigoma umejengeka katika utamaduni wa sehemu kuu mbili ambazo ni utamaduni wa Kigoma Mjini na wa nje ya mji. Mkoa wa Kigoma una kabila la Waha ambao wametamalaki katika maeneo mengi hususani nje ya wilaya ya Kigoma Mjini. Kwa upande wa Mjini, kuna makabila madogomadogo ambayo yote yanajumuishwa chini ya kabila moja la Wamanyema (Sovu, 2011). Tafiti zilizokwishafanywa kuhusu watu waishio Kigoma zinaonesha kuwa makabila haya yaliitwa Wamanyema kwa sababu ya kundi kubwa la wakazi wa mwanzo waliopita Kigoma kutoka Maniema huko Kongo. Watu hao walitoka Kongo kukimbia utawala mkali wa Wabelgiji (*Wabeleji* kama wanavyoitwa na baadhi ya wakazi wa Kigoma) ambao walikuwa wanatoka katika wilaya ya Maniema, mkoa wa Kivu, nchini Kongo. Katika kundi la Wamanyema kuna Wabwari, Wagoma, Wabembe, Wabondo, Wamasanze, Wakusu, Wabangubangu, Wanyekaramba na makabila mengineyo (KIDEA, 2001).

Kama tulivyofafanua hapo juu, lugha ya Kiha imetamalaki takribani katika wilaya zote saba za Mkoa wa Kigoma. Kiswahili cha Kigoma Ujiji kinazungumzwa zaidi katika maeneo ya mjini, hasa Ujiji, Bangwe, Kibirizi, Gungu na Mwanga (Sovu, 2011). Sovu anaeleza kuwa kutokana na shughuli

mbalimbali za kijamii, biashara, elimu na kutafuta kazi, baadhi ya watu wamekuwa wakihamahama kutoka katika maeneo ya vijijini na kwenda mjini. Ndani ya Manispaa ya Kigoma, Ujiji kumekuwa na mchanganyiko mkubwa wa makabila mbalimbali ya Waha, Wamanyema na makabila mengineyo kama Wahaya, Wanyakyusa, Wachaga, n.k. Lugha pekee wanayoweza kutumia katika mawasiliano ni Kiswahili. Kwa hivyo, raghba ya makala hii ni kubainisha tofauti za kifonolojia na kimsamiati baina ya Kiswahili cha Kigoma na Kiswahili sanifu na kuonesha jinsi lugha hizo zinavyoathiri mawasiliano fanisi.

### 1.4 Lugha ya Kiswahili Sanifu

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi inayotumika katika shughuli mbalimbali za kiutawala nchini Tanzania. Lugha hii imepewa kipaumbele kuliko lugha nyingine za makabila, kama vile Kiha, Kihaya, Kigogo, n.k. Kipaumbele hicho kinadhihirishwa kwa kuanzishwa kwa taasisi zinazokuza Kiswahili, kama vile Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA). Pia, Kiswahili kinatumika katika vyombo vya habari, shuleni na katika shughuli mbalimbali serikalini, hali iliyofanya lugha hii kukua na kutamalaki katika maeneo yote ya Tanzania (Hamad, 2018). Kiswahili sanifu ni kile ambacho kinatumika katika shughuli zote rasmi, kama vile ofisini, mikutanoni, mahakamani na bungeni. Katika makala hii tunarejelea kuwa Kiswahili sanifu ni kile kinachotokana na lahaja ya Kiunguja iliyosanifiwa na inayotumika katika kamusi na marejeleo mbalimbali. Kwa hivyo, makala hii imechunguza tofauti za kifonolojia na kimsamiati kati ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu ili kuona jinsi tofauti hizo zinavyoweza kuathiri mawasiliano fanisi miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili sanifu kama wafanyakazi wasio wenyeji wa mkoa wa Kigoma, wasafiri, wageni na wasomi.

## 2.0 Mkabala wa Kinadharia

Uchambuzi na uwasilishaji wa data za makala hii umeongozwa na Nadharia ya Isimu-historia na Linganishi. Nadharia hii iliasisiwa na William Jones mwaka 1786 alipolinganisha lugha za Kisankriti, Kigiriki na Kilatini ili kubaini uhusiano wa kimnasaba wa lugha hizo. Katika kuzilinganisha lugha mbili au zaidi ili kuona uhusiano wake kwa kutumia Nadharia ya Isimu-historia na Linganishi, wanaisimu hutumia mbinu maalumu ya kiulinganishi ijulikanayo kama Mbinu Linganishi. Kwa kutumia mbinu hii, lugha huchunguzwa katika vipengele mbalimbali vya kiisimu kama vile: msamiati wa msingi, fonolojia, mofolojia na sintaksia.

Mbinu Linganishi katika isimu linganishi hutumiwa kuchambua lugha mbili au zaidi ambazo zina asili moja ili kuonesha uhusiano wake wa kihistoria. Katika mbinu linganishi kuna vigezo vikuu vitatu vinavyotumiwa kulinganisha msamiati, mofolojia na fonolojia ya lugha zinazohusika. Kigezo cha kwanza ni msamiati wa msingi na cha pili ni kuchunguza visawe ili kuona kama lugha hizo

zina maneno yenye maana moja lakini yana maumbo tofauti. Kigezo cha tatu ni kukubaliana kwa sauti katika maneno kwa kulinganisha sauti za msamiati ili kuona ni kwa kiasi gani zinafanana au kutofautiana (taz. Massamba, 2007; 2017). Katika makala hii, kigezo cha tatu ndicho kilichotumika kuongoza uchambuzi wa data.

## 3.0 Metholodojia ya Uchunguzi

Makala hii imetokana na data za utafiti zilizokusanywa kwa kutumia mbinu za ushuhudiaji na mahojiano kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2023 katika mkoa wa Kigoma, Manispaa ya Kigoma, Ujiji. Maeneo yaliyofanyiwa utafiti yalikuwa kata za Ujiji, Mwanga, Gungu, Kibirizi na Bangwe. Data zilikusanywa kutoka kwa watoataarifa ambao walikuwa watu wa makamo (kuanzia miaka 60 na zaidi). Watoataarifa hao waliteuliwa kwa kuzingatia tajiriba na ukazi wa muda mrefu katika eneo la utafiti.

Data hizo zilirekodiwa kwa kinasasauti na kunukuliwa kwa maandishi na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu tano ambapo sehemu ya kwanza ni utangulizi na sehemu ya pili inahusu mkabala wa kinadharia uliotumika katika uchambuzi wa data za makala hii. Sehemu ya tatu inafafanua methodolojia iliyotumika kubainisha mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data. Aidha, sehemu ya nne ambayo ndiyo kiini cha makala hii, imejikita katika kubainisha tofauti za kifonolojia na kimofolojia baina ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili Sanifu. Nayo sehemu ya tano inatoa hitimisho la mjadala wa makala.

## 4.0 Tofauti baina ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili Sanifu

Sehemu hii inadhihirisha matokeo ya tofauti za kifonolojia na kimsamiati za watumiaji wa Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu.

### 4.1 Tofauti za Kifonolojia

Fonolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia mfumo wa sauti za lugha asilia za binadamu. (Massamba, 2010). Kwa mfano, fonolojia ya Kiswahili, Kiingereza, Kiha, Kihehe, Kilingala na ya Kinyamwezi. Baada ya ufafanuzi huo wa dhana ya fonolojia sasa tuchunguze tofauti za kifonolojia (Sovu, 2011). Kimsingi, tofauti za kifonolojia za Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu zimejibainisha katika namna mbili. Kwanza kuna tofauti katika matumizi ya sauti, yaani tofauti za uwakilishi wa kialfabeti na tofauti za matumizi ya urefushaji wa baadhi ya alfabeti.

#### 4.1.1 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti

Katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji baadhi ya sauti hutofautiana na Kiswahili sanifu katika utamkaji wa sauti hizo. Aghalabu sauti hizo ni zile zinazotokana na athari za maneno ya kigeni, kama vile sauti **[h], [bu], [mu]** na sauti zinazotokana na maneno ya Kibantu, kama vile sauti **[m], [n]**. Pia, sauti nyingine ni **[bh], [mu], [bu] na [tu],** [**ngo].** Kadhalika, utamkaji wa sauti **[r]** na **[l]** unabainisha zaidi

tofauti kati ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu. Tuchunguze kwa umakini tofauti hizo kama zinavyobainishwa katika sehemu zifuatazo:

#### 4.1.1.1 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [a] badala ya Sauti [ha]

Katika matumizi ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji, sauti [a] hutumiwa badala ya [ha] ambapo kuna aina fulani ya udondoshaji unaotokea. Kwa mujibu wa Massamba (2004), udondoshaji ni utaratibu wa kuondoa kipashio kimojawapo cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au sentensi. Huu ni utaratibu wa usemaji ambapo sauti au maneno fulani yasiyo muhimu sana kisarufi huweza kuachwa bila kuathiri maana iliyokusudiwa. Nao Matinde (2012) na Mgullu (1999) wanazumgumza kuhusu udondoshaji kwamba ni kuacha baadhi ya herufi katika neno. Katika lugha ya Kiswahili, baadhi ya lahaja katika matamshi yake huacha baadhi ya vitamkwa, jambo ambalo hutofautiana katika utamkaji wa maneno hayo na kuathiri umbo la neno bila kuathiri maana halisi ya neno hilo. Matamshi ya sauti hizi, yaani [a] na [ha] yanahusu maneno yote ya Kiswahili sanifu yanayoanza na sauti [h]. Mifano inayoonekana katika Jedwali Na. 1 linadhihirisha hoja hii:

**Jedwali Na. 1: Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [a] badala ya Sauti [ha]**

| Kiswahili cha Kigoma, Ujiji | Kiswahili Sanifu |
|---|---|
| a) **a**dithi | **ha**dithi |
| b) **a**bari | **ha**bari |
| c) **a**lali | **ha**lali |
| d) **a**endi | **ha**endi |
| e) **a**ji | **ha**ji |
| f) **a**po | **ha**po |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika mifano iliyopo kwenye Jedwali Na. 1, tunabaini kuwa baadhi ya wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji wanadondosha baadhi ya vitamkwa wanapozungumza ingawa watumiaji wa Kiswahili sanifu hutamka maneno hayo kwa usahihi. Mifano hiyo inabainisha kwamba baadhi ya fonimu au irabu zinazopatikana katika Kiswahili sanifu zinadondoshwa na watamkaji wa baadhi ya maneno katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji. Kama inavyoonekana katika data, sauti [h] hudondoshwa inapotokea katika mazingira kama hayo. Hata hivyo, udondoshaji wa sauti hiyo ya Kiswahili sanifu unatokana na kwamba sauti za Kiswahili cha Kigoma pengine hazikuathiriwa na sauti ya Kiarabu [h]. Badala yake kwenye sauti [h] huwekwa sauti [a]. Pia, huenda hali hii imetokana na kutagusana kwa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine.

#### 4.1.1.2 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [s] kuwa [sh]

Kuna tofauti ya utamkaji wa maneno baina ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu kupitia sauti [s]. Sauti hiyo hubadilika inapotamkwa na wasemaji

wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na kutamkwa kama [sh]. Tuchunguze mifano ifuatayo katika jedwali:

**Jedwali Na. 2: Tofauti za Mabadiliko ya Sauti [s] kuwa [sh]**

| **Kiswahili cha Kigoma, Ujiji** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| a) **sh**indikiza | **s**indikiza |
| b) **sh**indano | **s**indano |
| c) **sh**ikio | **s**ikio |
| d) gara**sh**a | gara**s**a |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika mifano kwenye Jedwali Na. 2 tunabaini kuwa wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma Ujiji wanatofautiana kimatamshi na wa Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu wasemaji wa Kiswahili sanifu huitamka sauti hiyo kama ilivyo, yaani [s] kwa baadhi ya maneno lakini kwa upande wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji sauti hiyo hubadilika na hutamkwa [sh], jambo ambalo huathiri utamkaji wa msamiati huo. Kwa mfano, katika neno *shindano* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji, neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Kiswahili sanifu hutamkwa *sindano*. Hivyo, dhana ya *sindano* kama kifaa chenye ncha kinachotumika kutilia dawa au kushonea nguo inakuwa tofauti na dhana ya neno *shindano* linalomaanisha kushindanisha vitu kwa lengo la kuchuana, kama vile michezo.

#### 4.1.1.3 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [r] badala ya [l]

Katika Kiswahili sanifu sauti [l] na [r] hutofautishwa katika matumizi yake na kusaidia kung’amua maana za maneno ya Kiswahili. Imebainika kuwa baadhi ya wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji hutumia sauti [r] badala ya [l] kama watumiavyo watumiaji wa Kiswahili sanifu. Mifano katika Jedwali Na. 3 inadhihirisha matumizi ya sauti hizo:

**Jedwali Na. 3: Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [r] badala ya [l]**

| **Kiswahili cha Kigoma, Ujiji** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| a) ku**r**a | ku**l**a |
| b) chaku**r**a | chaku**l**a |
| c) ra**r**a | la**l**a |
| d) pa**r**e | pa**l**e |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika mifano hapo juu, tunabaini tofauti ya matumizi ya sauti [r] na [l] ambapo mabadiliko ya sauti hizo huchangia kuathiri maana za msingi za Kiswahili sanifu. Kwa watumiaji wa Kiswahili sanifu, wanapoamiliana na watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji katika baadhi ya maneno, hukumbwa na utata wa kimaana za maneno. Ingawa katika muktadha wa matumizi huelewana, kwa kawaida maneno

hayo hutofautiana kimaana. Tuchunguze mifano hapa chini kutoka (BAKITA, 2015):

a) **L**a Ingiza mlo kinywani. Uk.554
b) Ku**r**a Uchaguzi huru aufanyao mtu ili kumpa mtu mwingine anayetaka dhamana ya
kushika wadhifa au madaraka fulani aghalabu ya uongozi Uk. 544
c) Chaku**l**a Kitu chochote ambacho watu na Wanyama hula, au ambacho mimea
hufyonza ili kendeleza Maisha na ukuaji wake.Uk. 113
d) Chaku**r**a Tafuta tafuta kitu kwa kukwaruza kama ambavyo hufanya kuku. Pia, vurugavuruga vitu vilivyowekwa au kupangwa kwa mpangilio ili kupata unachohitaji. Uk.113

Katika mifano hiyo tunabaini tofauti ya mabadiliko ya sauti [r] kuwa [l] yanayojitokeza kwa watu wa Kigoma wanapotamka maneno ya Kiswahili sanifu. Kwa hakika, mabadiliko hayo huathiri mawasiliano fanisi ya Kiswahili sanifu. Aidha, mabadiliko ya sauti [r] kuwa [l] yamebainishwa pia katika maeneo mengi ya Bara na hata ya pwani ya Tanzania. Mathalani, Massamba (2006) amebainisha tofauti hiyo katika Kimusoma na Kiswahili sanifu lakini pia akaonesha kuwa hata katika lahaja za mwambao wa pwani pia kuna matumizi ya kuchanganywa kwa sauti **/l/** na**/r/.** Kwa mfano, kuna wasemao *mshale* na wasemao *mshare*, wasemao *kulowa* na wasemao *kurowa* lakini ikumbukwe kuwa anapotamka *mshare* humaanisha *mshale* kama ilivyo katika Kiswahili sanifu. Hata hivyo, kwa mujibu wa Massamba (2006), utafiti zaidi unahitajika katika kuliweka bayana jambo hili hata katika maeneo ambayo hayajafanyiwa utafiti.

### 2.1.1.4 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [bh] badala ya [b]

Watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji hutumia sauti [bh] kama kibadala cha sauti [b] katika baadhi ya mazingira. Hali kama hii imebainishwa kuwa hujitokeza katika mazingira ambamo sauti [b] hufuatiwa na sauti [a]. Uchunguzi umebaini kuwa matamshi haya yanahusu maneno yote ya Kiswahili sanifu yenye sauti [b] yakifuatiwa na sauti [a] ama sauti hiyo iwe katikati ya neno au mwanzoni. Tuangalie mifano ifuatayo:

**Jedwali Na. 4: Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [bh] badala ya [b]**

| **Kiswahili cha Kigoma, Ujiji** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| a) e**bh**ana | bwana |
| b) sa**bh**a | saba |
| c) **bh**aba | baba |
| d) **bh**amia | bamia |
| e) **bh**aelezee | waelezee |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika Jedwali Na. 4 hapo juu, tunaona tofauti ya mabadiliko ya matumizi ya sauti [bh] na [b] baina ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu.

#### 4.1.1.5 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [mu] badala ya Sauti [m]

Katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji watumiaji husikika wakitamka sauti [mu] badala ya sauti [m]. Matamshi haya ya [mu] yanahusu pia maneno mengine ya Kiswahili sanifu yenye sauti [m] mwanzoni mwa neno. Tuchunguze mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 5:

**Jedwali Na. 5: Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [m] kuwa [mu]**

| Kiswahili cha Kigoma, Ujiji | Kiswahili Sanifu |
|---|---|
| a) **mu**ganga | **m**ganga |
| b) **mu**kulima | **m**kulima |
| c) **mu**zee | **m**zee |
| d) **mu**nyonge | **m**nyonge |
| e) **mu**kubwa | **m**kubwa |
| f) **Mu**swahili | **M**swahili |
| g) **mu**shenzi | **m**shenzi |
| h) **mu**jomba | **m**jomba |
| **i)** **mu**toto | **m**toto |
| **j)** **mu**sela | **m**sela |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Matumizi ya sauti [mu] kama yalivyobainishwa hapo katika Jedwali Na. 5, inaelekea kiasili Kiswahili sanifu ndicho kilichodondosha sauti [u] na kubakia na [m], jambo ambalo watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji inaelekea wameendelea kutumia katika asili ya lugha za Kibantu. Utokeaji wa hali hiyo pia umethibitishwa na Kihore na wenzake (2008) wanapoeleza kanuni ya udondoshaji *irabu ya kiambishi **mu-** inapofuatiwa na konsonati halisi*. Kihore na wenzake (*weshatajwa*) wanaendelea kufafanua kuwa kanuni hii ni ya msingi sana kwa upande wa Kiswahili kwani katika lugha nyingine za Kibantu haifanyi kazi. Hali hiyo imethibitika pia katika Kiha ambapo watumiaji wenye asili ya lugha hii hujikuta wanapotamka shurti waweke sauti [mu] kama tulivyobainisha katika Jedwali Na. 5 hapo juu. Hata hivyo, imebainishwa kuwa watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji husikika wakitamka [mu] badala ya sauti [m] ya Kiswahili sanifu. Hutamka hivyo kuonesha uelekeo au mahali kitu kilimo au mtu alimo, kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo katika jedwali:

**Jedwali Na. 6: Tofauti ya Matumizi ya Sauti [mu] Kuonesha Uelekeo wa Mahali**

| Kiswahili cha Kigoma, Ujiji | Kiswahili Sanifu |
|---|---|
| a) Saidi amekwenda **mu**mpira | Saidi amekwenda **m**pirani |
| b) Salome weka maji **mu**mtungi | Salome weka maji **m**tungini |
| c) Wazee wamekwenda **mu**mkutano | Wazee wamekwenda **m**kutanoni |
| d) Jumapili sisi hutembelea **mu**mbuga | Jumapili sisi hutembelea **m**bugani |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika mifano hapo juu tunabaini kuwa watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji husikika wakitamka [mu] badala ya sauti [m] ya Kiswahili sanifu. Kwa hakika, mabadiliko hayo hukusudiwa kuonesha uelekeo au mahali ambapo kitu kimo au mtu yumo.

#### 4.1.1.6 Tofauti ya Sauti [bu] au [tu] badala ya Sauti [wa]

Watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji hutamka sauti [bu] na [tu] badala ya sauti [wa]. Hivyo, husikika wakitamka *bule butoto* au *tule tutoto* badala ya *wale watoto.* Mazingira haya ya utamkaji wa sauti hii hutokea katika muktadha ambao matamshi haya yanayohusu maneno yote ya Kiswahili sanifu yenye sauti [wa] mwanzoni mwa neno. Tuchunguze mifano ifuatayo:

**Jedwali Na. 7: Tofauti ya Matumizi ya Sauti [bu]au [tu] badala ya Sauti [wa]**

| Kiswahili cha Kigoma, Ujiji | Kiswahili Sanifu |
|---|---|
| a) **bu**le butoto | **wa**le watoto |
| b) **bu**le **bu**ganga | **wa**le waganga |
| c) **bu**le **bu**ana siasa | **wa**le wanasiasa |
| d) **bu**le **bu**jamaa | **wa**le jamaa |
| **e)** **tu**le **tubata** | **wa**le bata |
| **f)** **tu**le **Tu**alimu | **wa**le **W**aalimu |
| **g)** **tu**le **tu**zee | **wa**le wazee |
| **h)** **tu**le **tu**dagaa | **wa**le dagaa |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika Jedwali Na. 7 hapo juu, tunabaini matumizi ya sauti [bu] na [tu] badala ya [wa], aghalabu huwa yanakusudia na kudhamiria juu ya masuala tofautitofauti. Inaweza kukusudia ama kudogosha, kuonesha dharau, kejeli au kusifia lakini sio maumbile ya mtu au mhusika mwenyewe vile alivyo. Hapa ina maana unaweza kusikia *bule bujamaa ni hatari sana* basi sio kuwa wanadhauriwa bali wanasifiwa juu ya ubora wa ujuzi au umahiri walionao juu ya jambo fulani.

#### 4.1.1.7 Tofauti ya Matumizi ya Sauti [-ga]

Watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji husikika wakitamka sauti [-ga] mwishoni mwa kitenzi, kama vile *kwenda**ga*** badala ya *kwenda* kwa Kiswahili

sanifu**.** Pia, imedhihirika kuwa hali hii haihusu kitenzi k*wend*a pekee bali vitenzi vingine vya Kiswahili sanifu. Mifano katika jedwali lifuatalo inadhihirisha:

**Jedwali Na. 8: Tofauti ya Matumizi ya Sauti [-ga]**

| **Kiswahili cha Kigoma, Ujiji** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| a) kwenda**ga** | huenda |
| b) penda**ga** | hupenda |
| c) cheza**ga** | hucheza |
| d) hapigagi | hapigi |
| e) hawaendesha**gi** | hawaendeshi |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika mifano kwenye Jedwali Na. 8, tunabaini matumizi ya sauti [-ga] katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji ambayo hayatumiki katika Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa uchunguzi huu [-ga] hutumiwa na watumiaji wachache wa Kigoma, Ujiji tofauti na sauti nyinginezo. Tumebaini kuwa kuna watumiaji wachache ambao hutumia sauti [-ga] ambayo inatoka katika lugha ya Kiha. Matumizi yake yametamalaki na hutumiwa sana na watu wa Kigoma. Kwa mujibu wa Sovu (2011), kuwapo kwa matumizi ya sauti [-ga] katika mazungumzo kumesababishwa na mwingiliano wa makabila uliosababisha kuwa na matumizi ya lugha mbalimbali kutoka mikoa mingine ya Tanzania. Aidha, hata nchi jirani zinazopakana na mkoa wa Kigoma zikiwamo Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Zambia kiasili baadhi zina sauti [-ga]. Mwingiliano huu pengine umeathiri hadi matumizi ya Kiswahili sanifu na hatimaye baadhi ya watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji nao hutumia sauti hiyo.

#### 4.1.1.8 Tofauti ya Mabadiliko ya Kialami [ngo] badala ya [eti]

Uchunguzi huu umebaini kuwa watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji hutumia sauti [ngo] badala ya [eti] ambayo hutumiwa na katika Kiswahili sanifu. Mifano katika jedwali lifuatalo inadhihirisha hilo:

**Jedwali Na. 9: Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [ngo] badala ya Sauti [eti]**

| **Kiswahili cha Kigoma, Ujiji** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| a) **Ngo!** Jamani huyu kijana amefaulu | Eti! Jamani huyu kijana amefaulu |
| b) **Ngo!** Wewe ni mwendawazimu? | Eti! Wewe mtoto ni mwendawazimu? |
| c) **Ngo!** Ee mama Salome umekula? | Eti! Ee mama Salome umekula? |
| d) **Ngo!** Amekuwa mbunge | Eti! amekuwa mbunge |
| **e)** **Ngo!** Amekufa | Eti! Amekufa |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika Jedwali Na. 9 hapo juu, tunabaini matumizi ya kialami [ngo!] katika Kiswahili cha Kigoma, badala ya [eti] kinachotumika katika Kiswahili sanifu. Uchunguzi unadhihirisha kuwa matumizi ya kialami **ngo!** kwa kawaida huwa yana uamilifu wa kuonesha mshangao wa kutaka kupata uhakika wa jambo, ingawa

katika Kiswahili sanifu [eti] humaanisha mshangao hususani inapotumiwa na alama ya mshangao (!).

### 4.1.2 Tofauti za Urefushaji Irabu

Massamba (2009) anaeleza kuwa katika Kiswahili sanifu urefushaji irabu huwa ni wa kufidia silabi. Hutokea pale ambapo hapo awali kulikuwa na irabu mbili tofauti zenye uamilifu tofauti kisilabi na moja kati yake ikadondoshwa au ikabadilika kuwa kiyeyusho kwa sababu za kimatamshi. Irabu inayobaki hurefushwa ili kufidia wakaa uliopotezwa na irabu iliyodondoshwa au iliyobadilishwa na kuwa kiyeyusho. Ingawa katika otografia ya Kiswahili irabu hiyo inayorefushwa huwa haioneshwi, kwa hakika, anaeleza kuwa imerefushwa. Baadhi ya mifano aliyoitoa ni hii ifuatayo:

| | Umbo | Matamshi | Maandishi ya Kiotografia |
|---|---|---|---|
| a) | mu+ana | [mwa:na] | mwana |
| b) | mu+alimu | [mwa:limu] | mwalimu |
| c) | mi-aka | [mya:ka] | miaka |
| d) | mu+ingereza | [mwi:ngereza] | mwingireza |
| e) | mu+ongo | [mwo:ngo] | mwongo |

**Chanzo:** Massamba (2009)

Katika mifano hapo juu tunabaini urefushaji wa irabu katika Kiswahili sanifu. Kwa kawaida, kwenye urefushaji wa sauti katika otografia ya Kiswahili, irabu inayorefushwa huwa haioneshwi. Massamba (2006) anaendelea kufafanua kuwa mbali na kurahisisha matamshi, urefushaji huo huwa hauna uamilifu mwingine. Katika makala hii imebainika kuwa watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji wana aina mbili za urefushaji wa irabu. Aina ya kwanza ni kama hiyo iliyoelezwa na Massamba (*keshatajwa*) kuhusu Kiswahili sanifu. Aina ya pili ni tofauti na hiyo ya kwanza na ina uamilifu mwingine kabisa. Huu ni urefushaji wa maneno mbalimbali ya Kiswahili sanifu. Urefushaji huu hufanyika katika irabu na una uamilifu wa kuonesha kutokujali au kusisitiza jambo ama kwa kulishangaa au la. Katika makala hii imebainika kuwa utumiaji huu umezoeleka katika mazungumzo yao ya kila siku. Mifano katika jedwali lifuatalo inadhihirisha matumizi hayo:

**Jedwali Na. 10: Urefushaji wa Irabu katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji**

| Kiswahili cha Kigoma, Ujiji | Kiswahili Sanifu | Urefushaji Irabu |
|---|---|---|
| a) ebh**aa**na | ebwana | ebwa:na |
| b) sa**aa**na | sana | sa:na |
| c) laal**a** | lala | la:la |
| d) nitol**eee** | nitolee | nitolee:e |
| e) mp**uuu**zi | mpuuzi | mpuu:zi |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Mifano katika Jedwali Na. 10 hapo juu, inaonesha kwamba kuna tofauti kati ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu katika urefushaji wa irabu.

Kiswahili cha Kigoma, Ujiji kina urefushaji ambao unachukua nafasi ya neno jingine ambalo lina maana sawa katika Kiswahili sanifu. Urefushaji huo unaweza kujitokeza katika aina mbalimbali za maneno kama vile vitenzi, vivumishi, nomino na aina nyingine za maneno. Katika vitenzi, urefushaji unajitokeza kwenye silabi ya mwisho ya neno lakini pia katika vivumishi urefushaji unajitokeza kabla ya silabi ya mwisho ya neno. Hata hivyo, urefushaji katika nomino unaweza kujitokeza katika silabi ya tatu ya neno. Vilevile, urefushaji huu unaonesha msisitizo wa aina fulani katika maneno yaliyorefushwa kama tulivyoona katika maneno *ebhaana*, *saaana*, *nimelaaaaa*, *nitoleee* na *mpuuuzi*.

### 4.1.3 Tofauti Zinazotokana na Lafudhi

Massamba na wenzake (2004) wanazungumza kuhusu lafudhi, kwa kueleza kwamba ni sifa ya kimasikizi inayohusiana na kusikika kwa sauti wakati wa kutamka matamshi ya mtu binafsi ambayo humpa msemaji utambulisho fulani ama wa kijamii au kieneo. Hapa wanamaanisha kwamba mazingira ya mtu yawe ya kijamii au kijiografia yanaweza kuleta athari za lafudhi kwa wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na wale watumiaji wa Kiswahili sanifu. Mtu yeyote anaweza kutambulika anatokea wapi kutokana na lafudhi yake, kwani watumiaji wa lugha huathiriwa na mazingira yao ya kijiografia. Katika muktadha huo, wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji wameathiriwa na mazingira yao na kusababisha kuwapo tofauti ya utamkaji baina yao na wale watumiaji wa Kiswahili sanifu. Tuangalie mifano ifuatayo kwa ufafanuzi zaidi.

**Jedwali Na. 11: Tofauti Zinazotokana na Lafudhi**

| Kiswahili cha Kigoma, Ujiji | Kiswahili Sanifu |
|---|---|
| a) kabechi | kabichi |
| b) stenti | stendi |
| c) susubika | susuwika |
| d) msinge | msingi |
| e) Ijumamosi | Jumamosi |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika mifano hapo juu tunabaini kwamba kuna tofauti za utamkaji wa maneno kwa wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na wale wa Kiswahili sanifu. Tofauti hiyo ni ile inayotokana na mazingira wanayoishi wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji ambayo huathiri usemaji katika Kiswahili sanifu. Usemaji huu unawatambulisha watumiaji wanaoishi eneo hilo kuweza kujulikana na watumiaji wa maeneo mengine.

## 4.2 Tofauti za Kimsamiati

Matokeo ya uchunguzi wa makala hii yanaonesha kwamba kuna tofauti za msamiati katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu. Kuna maneno ambayo yamebainika kutumika katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na si katika Kiswahili sanifu. Msamiati uliobainishwa hapa ni ule usio wa msingi. Msamiati

wa msingi ni aina ya msamiati ambao haubadilikibadiliki kutokana na mazingira. Kwa mfano, viungo vya maumbile ya mwanadamu kama vile *jicho*, *kichwa*, *sikio* pia vitu kama *mabonde*, *jua*, *mito* na *maziwa*. Uchunguzi wa makala hii umebaini kuwa msamiati usio wa msingi ni ule ambao unahusu vitu vingine ambavyo sio hivyo vilivyotajwa.

Watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji husikika wakitumia msamiati ambao hautumiwi na watumiaji wa Kiswahili sanifu. Msamiati wa aina hii ni mwingi na unahusu aina za vyakula, samaki, mbogamboga na majina ya vitu mbalimbali. Baadhi ya msamiati huo unadhihirishwa katika jedwali kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 12: Tofauti za Msamiati Unaotokana na Nomino za Vitu mbalimbali**

| **Kiswahili cha Kigoma, Ujiji** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| a) mkubi | majani ya maharage |
| b) msusa/msoma | majani ya maboga |
| c) kirindaa | sufuria kubwa la kupikia mchele |
| d) makira | wavu wa kuvulia samaki/kokoro |
| e) mgazi | mchikichi |
| f) shashee/kamwanyaa | mfuko wa nailoni/plastiki |
| g) kanyaro | majivuno/Hali ya kujidai |
| h) kiparata | kadi ya mpigakura |
| i) mbambulaa | jiko la kupikia |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika msamiati uliodokezwa hapo juu imebainika kuwa kuna msamiati mwingi wa majina ya vitu mbalimbali. Vilevile, uchunguzi huu umedhihirisha kuwa kuna tofauti za msamiati unaotokana na vitenzi mbalimbali vya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu. Jedwali lifuatalo linadhihirisha:

**Jedwali Na. 13: Tofauti za Msamiati Unaotokana na Vitenzi mbalimbali**

| **Kiswahili cha Kigoma, Ujiji** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|
| a) zovya | vuruga/lulunganya |
| b) dabua | danganya/ongopea mtu |
| c) parua | paa/para |
| d) hombora | saidia/okoa |
| e) tobhanga | haribu |
| f) zebheza | bababaisha |
| g) dikira | vamia |
| h) chakiza | vua samaki |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2023)

Katika Jedwali Na. 13 hapo juu tunabaini tofauti za kimsamiati baina ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu. Katika data hii imebainika kuwa msamiati tulioudhihirisha hapo juu katika Jedwali Na. 12 na 13 umetokana na athari ya mwingiliano wa jamii ya Kigoma, Ujiji na jamii nyingine za nje ya Kigoma. Kwa

sababu kuna baadhi ya athari zinatokana na mwingiliano wa lugha za jamii kama vile Kiha, Kibembe, Kirundi na lugha za kigeni kama vile Kifaransa, Kiarabu na hata Kiingereza. Hebu tuchunguze jedwali lifuatalo hapo chini:

**Jedwali Na.14: Mifano ya Msamiati wa Kiswahili cha Kigoma Ujiji na Asili zake**

| **Msamiati wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji** | **Matamshi katika Lugha ya Asili** | **Lugha Husika ya Asili** |
|---|---|---|
| a) mkubi | *umukhubhi* | Kiha |
| b) msoma | *umusoma* | Kiha |
| c) senya | *ugushenya* | Kiha/Kirundi |
| d) tengasi | *intengasi* | Kiha |
| e) kirindaa | *elendaa* | Kibembe |
| f) shashee | *sache/sachet* | Kifaransa/Kiingereza |
| g) kuhomba | *uguhomba* | Kiha |
| h) kazovya | *kazovya* | Kimasanze/Kibwari |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2023)

Katika Jedwali Na. 14 hapo juu, tumebaini kwamba baadhi ya maneno tunayoyasema kuwa ni Kiswahili cha Kigoma, Ujiji, kietimolojia yanatokana na lugha za Kiha, Kifaransa, Kibembe na Kimasanze, pengine na lugha nyinginezo. Hivyo, kama utafanyika utafiti wa kuchunguza etimolojia, tunaweza kubaini etimolojia za maneno hayo kwa utondoti zaidi. Kwa mintarafu hii, hali hiyo inadhihirisha bayana kwamba Kiswahili cha Kigoma, Ujiji kimeathiriwa na mwingiliano wa lugha hizo kama ilivyobainishwa hapo juu.

Kwa ujumla, watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji huwa hawabaini kuwa Kiswahili wanachokitumia ni tofauti na Kiswahili sanifu kilichozoeleka katika maeneo mengine ya nje ya Kigoma. Mathalani, matumizi ya msamiati kama vile *kibombobombo* huwachangaya watumiaji wengine hasa wanaotoka maeneo ya pwani ambapo wao hutumia neno *kunguru*. Uchunguzi umebaini kuwa hata watumiaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji wanapokwenda katika maeneo mengine nje ya Kigoma hupata shida ya mawasiliano kwa baadhi ya maneno.

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba kuna tofauti nyingi za kifonolojia na kimsamiati katika Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu. Imebainishwa kwamba kuna athari mbalimbali za kifonolojia ambazo hutokea katika matamshi ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji zinazotofautiana na Kiswahili sanifu. Miongoni mwa athari hizo ni mabadiliko ya sauti, udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa sauti pamoja na tofauti za lafudhi.

Aidha, tumebainisha tofauti za msamiati usio wa msingi unaohusu majina na vitenzi mbalimbali. Tofauti hizi zinafanya wale wasiokuwa wakazi wa eneo hilo kutopata maana halisi ya msamiati unaotamkwa, hivyo, huchangia athari ya mawasiliano. Kwa ujumla, tofauti zilizobainika katika msamiati huo zinaonesha tofauti za matamshi lakini pia ndani ya matamshi hayo yanaonekana maumbo ya

maneno ambayo yamechangia kutofautisha Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu.

**5.0 Hitimisho**

Kwa ujumla, shabaha ya makala hii ilikuwa kuchunguza tofauti za kifonolojia na kimsamiati baina ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji na Kiswahili sanifu ili kubaini tofauti hizo zinavyojitokeza na kuathiri ufanisi wa mawasiliano. Tumeweza kubaini kuwa athari za kifonolojia zitokanazo na matamshi ya Kiswahili cha Kigoma, Ujiji yanatofautiana na Kiswahili sanifu. Pia, kuna tofauti ya msamiati usio wa msingi unaotokana na majina ya vitu na vitenzi. Aidha, makala hii imebainisha kuwa kwa wageni wanaoingia katika mkoa wa Kigoma kunaweza kuwa na athari za mawasiliano, kutokana na fonolojia ya matamshi na msamiati mbalimbali wa lugha hizi. Hivyo, pamoja na tofauti hizo katika msamiati, pia kuna mfanano ambao kwa kiasi kikubwa msamiati huo unafanana kimaana. Hapa ni kwamba maana ya msamiati unaozungumzwa na wasemaji wa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji unafanana kimaana na ule ambao unatamkwa na wasemaji wa Kiswahili sanifu. Kwa mintarafu ya makala hii, kuna maswali mbalimbali ambayo tunaweza kujiuliza kama vile: ni kwa sababu gani Kiswahili cha Kigoma, Ujiji kinatofautiana sana na Kiswahili sanifu? Je, tofauti hizo zinaweza kubainishwa katika vipengele vingine kama vile vya kimuundo, mtindo na maana? Je, ni kweli kwamba Kiswahili cha Kigoma, Ujiji kinaweza kutofautiana na Kiswahili cha maeneo mengine ya Kigoma? Kudhihirika kwa maswali haya ni wazi kuwa bado tafiti nyingine zinahitajika ili kubainisha sababu mbalimbali za tofauti hizo. Aidha, kwa kuwa utafiti huu umedokeza kuwa Kiswahili cha Kigoma, Ujiji kina athari za lugha za makabila kama Kiha, Kirundi, Kibembe na lugha nyinginezo za Kibantu, hilo linaashiria kuibuka kwa lahaja nyingine ya Kigoma, Ujiji hususani katika maeneo haya ya Tanzania Bara. Hivyo, mwandishi anapendekeza tafiti zaidi zifanyike ili kuyapatia majibu maswali hayo.

## Marejeleo

Antilla. R. (1972). *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*. Macmillan: Universityof California.

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Besha, R.M. (1974). "Mwingiliano kati ya Lugha". *Mulika*. 6: 15-32.

Gumperz, J. (1968). "The Speech Community in Duranti". *Linguistic Anthropology*. 1: 66-73.

Hamad, K.T. (2018). Tofauti za Msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

John, W. (1786). *Language Classification, History and Method*. Cambridge: Cambridge University Press.

Juma, U.S. (2021). Ulinganishi wa Kiisimu baina ya Kipemba na Kingazija. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

KIDEA, (2001). *The Baha and Related people of Kigoma Region. History, Tradition, Culture and Development*: Dar es Salaam: Tanzania Printing Limited.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: KIUTA.

Luka, A. (2012). "Mwingiliano wa Matumizi ya Lugha baina ya Kiswahili na Kimeru na Athari zake katika Lugha hizi." Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maganga, C. (2008). "Juhudi za Ukuzaji wa Kiswahili Tanzania Bara." Katika J.G. Kiango (Mh.), *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Kur. 22-37.

Massamba, D.P.B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Massamba, D.P.B., Kihore Y.M. na Hokororo, J.I. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA), Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2010). *Phonological Theory, History and Development.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2017). *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100KK hadi 2000BK.* Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.

Massamba, D.P.B. (2006). Kiswahili cha Musoma, Mwanzo wa Lahaja Nyingine? *Kiswahili*. 69: 37-51.

Massamba, D.P.B. (2007). *Kiswahili Origins and The Bantu Divergence-Convergence Theory.* Dar es Salaam: TUKI.

Maganga, C. (1997). *Historia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Masebo, J.A. na Nyangwine, N. (2008). *Nadharia ya Lugha. KISWAHILI 1*. Kidato cha 5 na 6. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Mathooko, P.M. (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njiku Books.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mekacha, R.D.K. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Minocity: Chuo Kikuu cha Taaluma za Kigeni cha Osaka.

Mdee, S.J. (2014). *OSW 613: Isimu Jamii*. Dar es Salaam: KIUTA.

Mgullu, R.S. (2001). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Msanjila, Y.P., Kihore, Y. na Massamba, D.P.B. (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Nurse, D. na Spear, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing The History and Language of an African Society, 800-1500*. Philadephia: University of Pennsylvania Press.

Nyanda, J. (2015). Athari za Lugha ya Kinyamwezi katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. Tazmili ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sovu, A.Y. (2011). Matumizi ya Kiha katika Kiswahili cha Mazungumzo. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Pili). Nairobi: Oxford University Press.

Wenceslaus, M. (2015). Athari za Lugha ya Kijita katika Kujifunza Kiswahili. Tazmili ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.